Hizi ajali zinaweza kuepukika kwa urahisi. Kutoendesha gari ukiwa mlevi kunaweza kuokoa maisha.

- Usikunywe pombe ikiwa unajua utahitaji kupeleka gari baadaye.
- Ukipanga kukunywa pombe, jua mapema vile utafika nyumbani.
- Omba mtu ambaye sio mlevi akuendeshe nyumbani.
- Ambia marafiki na wanafamilia wasiendeshe gari wakiwa walevi.
- Usiruhusu kuendeshwa au watoto wako kuendeshwa na dereva anayeweza kuwa mlevi.

Usiwahi Kuwaacha Watoto Peke Yao Ndani ya Gari

Kuwaacha watoto peke yao ndani ya gari au kuwaacha watoto peke yao karibu na gari ambalo halijafungwa kunaweza kuwa hatari sana.

- Watoto wanaweza kupata joto haraka ndani ya gari. Kupata joto ni moja ya sababu kubwa za vifo vya watoto chini ya umri wa miaka 14 vinavyohusiana na magari na hasa hatari katika joto la Arizona.
- Usiwaache watoto peke yao ndani ya gari injini ikiwa imewashwa au ufunguo ukiwa ndani ya gari. Hii inaweza kusababisha ajali ambapo gari linaweza kubingirika watoto wako wakiwa ndani yake.
- Watoto wanaowachwa peke yao karibu na gari ambalo halijafungwa wanaweza kujifungia ndani ya gari au buti la gari.

Hizi ajali zinaweza kuepukwa kwa urahisi.

- Usiwahi kumuacha mtoto wako peke yake ndani ya gari, hata ikiwa unatarajia kurudi haraka.
- Usiwahi kuwacha injini ikiwa imewashwa au kuwacha funguo zako ndani ya gari.
- Weka vitu muhimu kama vile simu, pochi, au mkoba kando ya mtoto anayelala ili usisahau kwamba ako hapo.
- Wafunze watoto wako kutocheza ndani, chini, au karibu na magari.
- Ukimuona mtoto ndani ya gari ambalo limefungwa, piga simu kwa 9-1-1.

Uvukaji Barabara

Ni muhimu pia kuwa salama ukiwa karibu na magari hata wakati huendeshi. Wafunze wanafamilia wako kuhusu jinsi ya kuvuka barabara kwa usalama na hakikisha wamekuza hizo tabia nzuri.

- Kabla ya kuvuka barabara, angalia kulia na kisha kushoto kwa magari yanayokuja.
- Vuka barabara katika sehemu maalum zilizoteuliwa kuvukia barabara.
- Wafunze watoto wako kutovuka barabara bila kushikiliwa mkono na mtu mziwa wanayemuamini.
- Kuwa makini katika maeneo ya uegezaji magari na njia za binafsi za kwenda nyumbani.

Arizona Department of Health Services

Kuwa Salama Karibu na Magari

Programu ya Afya ya Wakimbizi
Idara ya Huduma za Afya ya Arizona

Tii Sheria za Barabarani

Njia moja rahisi kabisa kupunguza uwezekano wako wa kujeruhiwa ukiendesha gari ni kutii sheria za barabarani na uendeshe kwa usalama iwezekanavyo.

- Fuata viwango vya kasi.
- Simama katika taa nyekundu na vibao vya barabarani vya kusimama.
- Epuka mambo yanayo kuzubaisha unapoendesha gari.
- Usifuate gari lingine lililombele yako karibu sana.

Tumia Mikanda ya Usalama ya Viti

Hata unapoendesha gari kwa uangalifu, huwa kuna uwezekano wa ajali kutokea. Ni muhimu kuwa tayari, na njia moja ya kufanya hivi ni kwa kujifunga mkanda wa usalama wa kiti wakati wote unapondesha gari. Jambo hili ni muhimu kwa sababa:

- Mikanda ya usalama ya viti huokoa maelfu ya maisha kila mwaka.
- Mikanda ya usalama ya viti hupunguza uwezekano wa majeraha unapopata ajali ya gari.
- Katika jimbo la Arizona, kuvaa mkanda wa usalama wa kiti ni sheria. Ikiwa wewe au abiria wako hamjavaa mikanda ya usalama ya viti, utahitajika kulipa faini.

Pia ni muhimu kuhakikisha kwamba unavaa mkanda wako wa usalama wa kiti vizuri.

- Mkanda wa usalama wa kiti unafaa kupitia mapaja yako na mkanda wa bega unafaa kupitia kifua chako.
- Usivae mkanda wa bega chini ya mkono, nyuma ya mgongo, au kwenye shingo. Hii inaweza kusababisha majeraha mabaya ikiwa utakuwa katika ajali.
- Mkanda haufai kulegea. Hakikisha kwamba watoto hawachezi na mikanda yao ya usalama ya kiti au kuilegeza.

Usalama wa Kiti cha Gari

Watoto walio wadogo sana kutumia mikanda ya kawaida ya usalama ya viti wanafaa wawekwe katika kiti maalum cha gari. Kuchagua kiti kinachofaa cha gari ni muhimu kwa usalama wa mtoto wako.

- Kutumia kiti cha gari kisichofaa kunaweza kuwa hatari. Hakikisha kiti chako cha gari kimeundiwa umri, urefu, na uzito wa mtoto wako.
- Kulingana na sheria ya Arizona, lazima watoto wote walio chini ya umri wa miaka 8 na wenye urefu wa 4’9” au wafupi zaidi wawe katika kiti cha gari au kiti nyongeza.
- Tumia chati iliyo upande wa kulia kujua aina ya kiti cha gari mtoto wako anahitaji.

Unapopata kiti kinachofaa, ni muhimu kukifunga ipasavyo na kumkalisha mtoto vizuri.

- Hakikisha kwamba lijamu na hatamu inabana kwenye kifua cha mtoto wako.
- Hakikisha bakoli na klipu ya kifua imefungwa.
- Ikiwa huna uhakika jinsi ya kutumia kiti cha gari, uliza usaidizi na nyenzo zaidi kutoka kwa uajenti wako wa uhamiaji.

Usiwahi Kupeleka Gari Ukiwa Mlevi

Kuendesha gari ukiwa mlevi au ukiwa umetumia madawa ya kulevya sio salama na kunaweza kuwaweka wewe na abiria wako katika hatari ya majeraha mabaya.

- Mamia ya watu hufa kila mwaka kwa sababu ya ajali zinazosababishwa na madereva walevi
- Uendeshaji gari ukiwa mlevi ni kinyume na sheria na kutasababusha ulipe faini au ufungwe jela